FUNZO LA 29

1. Je, Waisraeli waliamini Neno la Mungu, kuwa Mungu alinena na Musa?
-Ndiyo.

2. Je, ikiwa hatutaamini Neno la Mungu, tunamuitaje Mungu?
-Muongo.

3. Je, Mungu atawaokoa wasioamini Maneno ya Mungu?
-La.

4. Farao alisema nini Musa alipomwambia kuwa Bwana amemwamuru awaachilie Waisraeli?
-Farao alisema "Simjui Bwana, na sitawaachilia Waisraeli."

5. Je, Mungu alijua kuwa Farao hatawaruhusu Waisraeli watoke Misri?
-Ndiyo.
-Mungu anajua kila kitu kitakachofanyika kabla kifanyike.

6. Je, kwa nini Mungu aliamua kuonyesha nguvu zake kuu kwa Farao na Wamisri?
-Ili wajue kuwa yeye pekee ndiye Mungu wa kweli.

7. Je, Mungu alionyeshaje nguvu zake kuu kwa Waisraeli na Wamisri?
-Mungu alituma mapigo makubwa kwa Farao na Wamisri.

8. Hayo mapigo yalikuwa gani?



-Mungu alibadilisha maji ya mto kuwa damu.
-Mungu alituma vyura kuwasumbua Wamisri.
-Mungu alituma chawa kuwauma Wamisri.
-Mungu alituma nzi kuwauma Wamisri.

-Mungu aliwaua wanyama wote wa Wamisri.
-Mungu alituma majipu ili kuwapa Wamisri uchungu.
-Mungu alituma mvua ya mawe ili kuharibu mimea ya Wamisri.
-Mungu alituma nzige ili wale mimea ya Wamisri.
-Mungu alituma giza totoro ili Wamisri wasione.

9. Je, Farao alisema nini kila wakati Mungu alipotuma pigo?
-Farao alimwambia Musa kuwa atawaruhusu Waisraeli waondoke.

10. Je, Farao alifanya nini kila wakati Mungu alipoondoa pigo?
-Farao alikataa kuwaruhusu Waisraeli waondoke.

11. Je, kwa nini mapigo hayakufika katika sehemu ambayo Waisraeli waliishi?
-Kwa sababu Mungu aliahidi Ibrahamu, Isaka na Yakobo kuwa atawabariki na kuwafanya kuwa watu wengi.
-Kwa sababu Mungu alikuwa akionyesha Farao, Wamisri na Waisraeli kuwa yeye ndiye Mungu pekee na hakuna mwingine.

12. Je, nini kitakachowafanyikia wale wanaopigana dhidi ya Mungu?
-Mungu atawaharibu.

-Ingawaje Mungu alituma mapigo tisa makali, je, Farao aliwaruhusu Waisraeli waondoke?
-La.

-Je, Mungu alijua kuwa Farao hatawaruhusu Waisraeli waondoke?
-Ndiyo.

-Mungu alijua kuwa Farao hatawaruhusu Waisraeli waondoke.

-Hata kabla Mungu amchague Musa kuwaongoza Waisraeli, Mungu alijua kuwa Farao atakataa kuwaruhusu Waisraeli kuondoka.

-Mungu anajua kila kitakachofanyika kabla kifanyike.

-Je, Farao anaweza pigana dhidi ya Mungu na ashinde?
-La.

-Je, yeyote anaweza pigana dhidi ya Mungu na ashinde?
-La.

-Haijalishi watakachosema watu, hawawezi kuzuia kazi ya Mungu.

-Haijalishi watakachofanya watu, hawawezi kuzuia kazi ya Mungu.

-Mungu akiamua kufanya jambo, lazima atatimiza.



-Mungu atatuma pigo moja kisha Farao atawaruhusu Waisraeli waondoke.

Tusome Kutoka 11:1

1-Bwana akamwambia Musa, Liko pigo moja bado, nitakaloleta juu ya Farao na juu ya Misri; baadaye atawapa ninyi ruhusa mtoke huku; naye hapo atakapowapa ruhusa, atawafukuza mtoke huku kabisa kabisa.

-Je, pigo la mwisho ambalo Mungu alituma ni lipi?

Tusome Kutoka 11:4-7

4-Musa akasema, Bwana asema hivi, Kama usiku wa manane mimi nitatoka nipite kati ya Misri;
5-na wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri watakufa, tangu yule mzaliwa wa kwanza wa Farao aketiye katika kiti chake cha enzi, hata mzaliwa wa kwanza wa huyo kijakazi aliye pale nyuma ya jiwe la kusagia; na wazaliwa wa kwanza wote wa wanyama.
6-Ndipo kutakuwa na kilio kikuu katika nchi yote ya Misri, ambacho mfano wake haujakuwa bado majira yo yote, wala hautakuwako mfano wake tena kabisa.
7-Lakini katika wana wa Israeli hapana hata mbwa atakayetoa ulimi juu yao, juu ya mtu wala juu ya mnyama; ili kwamba mpate kujua jinsi Bwana anavyowatenga Wamisri na Waisraeli.

-Pigo la mwisho litawaua wazaliwa wa kwanza wa Wamisri na mifugo yao.

-Kwa sababu pigo la mwisho lilikuwa kali zaidi, Mungu aliwaamuru Waisraeli wajiandae.

-Kwa sababu pigo la mwisho lilikuwa kali zaidi, je, Mungu aliwaamuru Waisraeli wafanye nini ili wazaliwa wao wa kwanza wasife?

Tusome Kutoka 12:1 & 3-5

1-Bwana akanena na Musa na Haruni katika nchi ya Misri, akawaambia,
3-Semeni na mkutano wote wa Israeli, mkawaambie, Siku ya kumi ya mwezi huu kila mtu atatwaa mwana-kondoo, kwa hesabu ya nyumba ya baba zao, mwana-kondoo kwa watu wa nyumba moja;
4-na ikiwa watu wa nyumba ni wachache kwa mwana-kondoo, basi yeye na jirani yake aliye karibu na nyumba yake na watwae mwana-kondoo mmoja, kwa kadiri ya hesabu ya watu; kwa kadiri ya ulaji wa kila mtu, ndivyo mtakavyofanya hesabu yenu kwa yule mwana-kondoo.
5-Mwana-kondoo wenu atakuwa hana ila, mume wa mwaka mmoja; mtamtwaa katika kondoo au katika mbuzi.

-Je, Mungu aliamuru kila jamii ya Israeli ifanye nini ili wazaliwa wao wa kwanza wasife?

-Wachague kondoo au mbuzi wa mwaka mmoja.



-Je, ni aina gani ya kondoo au mbuzi ambayo Mungu aliwaamuru wachague ili wazaliwa wa kwanza wasife?

-Asiye na mawaa.

-Je, kwa nini Mungu aliamuru kuwa huyo kondoo au mbuzi wa mwaka mmoja asiwe na mawaa?

-Kwa sababu Mungu ni mkamilifu.

-Kwa sababu kila anachosema Mung ni kikamilifu.
-Kwa sababu kila anachofanya Mungu ni kikamilifu.

-Mungu angekubali kondoo au mbuzi wa mwaka mmoja asiye na mawaa peke yake.

-Mungu hawezi kubali sadaka mgonjwa.
-Mungu hawezi kubali sadaka iliyoumia.

-Je, unakumbuka yule kondoo wa kiume aliyefungwa kwa pembe ambaye alichukuwa nafasi ya Isaka?

-Je, kwa nini huyo kondoo alifungwa kwa pembe?

-Kwa sababu Mungu ni mkamilifu.
-Kwa sababu Mungu atakubali sadaka kamilifu tu.

-Ikiwa Waisraeli wangeokolewa kutoka kwa kifo, je, wangeitajika kuwa makini kufanya nini?

-Kumtii Mungu.

-Na wachague kondoo au mbuzi wa kiume wa mwaka mmoja.

-Je, nini kingine ambacho Mungu aliwaamuru?

Tusome Kutoka 12:6

6-Nanyi mtamweka hata siku ya kumi na nne ya mwezi ule ule; na kusanyiko lote la mkutano wa Israeli watamchinja jioni.

-Je, Mungu aliwaamuru kumuhifadhi huyo kondoo kwa muda gani?

-Hadi siku ya kumi na nne ya mwezi.

-Katika siku ya kumi na nne, Mungu aliwaamuru Waisraeli wamfanyie nini yule kondoo?

-Mungu aliamuru kuwa kondoo lazima auawe.
-Mungu aliamuru kuwa kondoo lazima afe.

-Je, kwa nini Mungu aliamuru kuwa kondoo lazima afe?

-Hii ilikuwa ili kuwafundisha Waisraeli kuwa adhabu ya dhambi ni kifo.

-Kabla ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, kifo hakikuwa duniani.



-Kwa sababu Adamu na Hawa walitenda dhambi, kifo kiliingia duniani.

-Kwa sababu Adamu na Hawa walitenda dhambi, kifo kiliingia kwa watu wote.

-Je, Mungu aliwaamuru Waisraeli wafanye nini na damu ya yule kondoo?

-Waiteke kwa bakuli.

-Ikiwa Waisraeli wataokolewa kutokana na kifo, ni lazima wawe makini kutii amri ya Mungu.

-Na wamuue yule kondoo au mbuzi wa mwaka mmoja na kuteka damu yake katika bakuli.

-Je, Mungu aliwaamuru wafanyie nini ile damu watakoyoteka katika bakuli?

Tusome Kutoka 12:7

7-Nao watatwaa baadhi ya damu yake na kuitia katika miimo miwili na katika kizingiti cha juu, katika zile nyumba watakazomla.

-Mungu aliwaamuru Waisraeli kwamba, wapake ile damu katika vizingiti vya mlango, upande wa juu na pande mbili za kando, katika kila nyumba ambapo yule mbuzi angeliwa.

-Ile damu ndiyo ambayo ingewaokoa Waisraeli kutokana na kifo.

-Ikiwa Waisraeli wataokolewa kutokana na kifo, ni lazima wawe makini kutii amri ya Mungu.

-Na wapake ile damu katika vizingiti vya mlango, upande wa juu na pande mbili za kando, katika kila nyumba ambapo yule mbuzi angeliwa.

-Je, Mungu aliwaamuru Waisraeli wafanye nini tena?

Tusome Kutoka 12:22b

22-Tena mtu ye yote miongoni mwenu asitoke mlangoni mwa nyumba yake hata asubuhi.

-Mungu aliwaamuru Waisraeli kukaa katika nyumba iliyopakwa damu hadi asubuhi.

-Waisraeli walistahili kukaa ndani na damu nje.

-Je, kwa nini Mungu aliamuru Waisraeli wawe ndani na damu iwe nje?

-Damu nje ilipaswa kuwafunika Waisraeli walio ndani.

-Kifo cha kondoo nje, kilipaswa kuwafunika Waisraeli ndani.

-Ikiwa Waisraeli wataokolewa kutokana na kifo, ni lazima



wawe makini kutii amri ya Mungu.

-Na wakae katika nyumba iliyopakwa damu hadi asubuhi.

-Je, Mungu aliwaamuru Waisraeli wafanye nini tena?

Tusome Kutoka 12:46b

46-Wala msivunje mfupa wake uwao wote.

-Mungu aliwaamuru Waisraeli wasivunje mfupa wowote wa yule kondoo.

-Ikiwa Waisraeli wataokolewa kutokana na kifo, ni lazima wawe makini kutii amri ya Mungu.

-Na wasivunje mfupa wowote wa yule kondoo.

-Mungu aliwaamuru Waisraeli wafanye kila kitu jinsi alivyowaamuru.

-Je, ikiwa Waisraeli hawangefanya kila kitu kama alivyowaamuru Mungu, nini kingewafanyikia?

-Lile pigo lingekuja kwao na wazaliwa wao wa kwanza wangekufa pia.

-Mungu angeokoa wazaliwa wao wa kwanza iwapo wangetii kufanya kila kitu alivyowaamuru.

-Mungu angeokoa wazaliwa wa kwanza wa Israeli kama wangefuata njia ya Mungu.

-Je, Mungu atatruhusu kujiokoa katika njia yetu?
-La.

-Je, ni njia ya nani pekee ambayo itatuokoa?
-Njia ya Mungu.

-Je, nini kiliwafanyikia Adamu na Hawa walipofuata njia yao na kujitengenezea mavazi kutoka kwa majani ya miti?

-Mungu alikataa mavazi yao.

-Je, nini kilimfanyikia Kaini alipofuata njia yake na kukataa kutoa sadaka jinsi Mungu alivyokuwa amesema?

-Mungu alikataa kafara ya Kaini.

-Njia ya Mungu pekee ndiyo itakayotuokoa.
-Kama hatutafuata njia ya Mungu, Mungu atatukataa.

-Je, Mungu aliwaahidi nini Waisraeli iwapo wangemtii?

Tusome Kutoka 12:12-14

12-Maana nitapita kati ya nchi ya Misri usiku huo, nami nitawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, wa mwanadamu na wa mnyama; nami nitafanya hukumu juu ya miungu yote ya Misri; Mimi ndimi Bwana.



13-Na ile damu itakuwa ishara kwenu katika zile nyumba mtakazokuwamo; nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu, lisiwapate pigo lo lote likawaharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri.

14-Na siku hii itakuwa ukumbusho kwenu, nanyi mtaifanya iwe sikukuu kwa Bwana; mtaifanya iwe sikukuu katika vizazi vyenu vyote, kwa amri ya milele

-Iwapo Waisraeli wangemtii Mungu, Mungu aliwaahidi nini?

-Mungu aliwaahidi kuwa hilo pigo halingekuja kwao na wazaliwa wao wa kwanza hawangekufa pia.

-Je, Waisraeli walimtii Mungu?

Tusome Kutoka 12:28

28-Basi wana wa Israeli wakaenda na kufanya mambo hayo; vile vile kama Bwana alivyowaamuru Musa na Haruni, ndivyo walivyofanya.

-Waisraeli walifanya kwa hakika kila kitu ambacho Mungu aliwaamuru kufanya.

-Je, kama mmoja wa Israeli angechagua kondoo mgonjwa, Mungu angemwokoa?
-La.

-Je, kama mmoja wa Israeli angemfunga kondoo badala ya kumuua, je, Mungu angemwokoa?

-La.

-Kondoo alipaswa kufa.
-Damu ya kondoo ilipaswa kumwagika.

-Mungu hakutaka Waisraeli wasahau kuwa adhabu ya dhambi ni kifo.

-Je, nini kilichofanyika usiku huo?

Tusome Kutoka 12:29-30

29-Hata ikawa, usiku wa manane Bwana akawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, tangu mzaliwa wa kwanza wa Farao aliyeketi katika kiti chake cha enzi, hata mzaliwa wa kwanza wa mtu aliyefungwa katika nyumba ya wafungwa; na wazaliwa wa kwanza wote wa wanyama.
30-Farao akaondoka usiku, yeye na watumishi wake wote, na Wamisri wote; pakawa na kilio kikuu katika Misri; maana hapakuwa na nyumba hata moja asimokufa mtu.

-Mzaliwa wa kwanza wa Farao na wazaliwa wa kwanza wa Wamisri walikufa.

-Mzaliwa wa kwanza wa mifugo ya Farao na wazaliwa wa kwanza wa mifugo ya Wamisri walikufa.

-Je, Mungu aliwaua wazaliwa wa kwanza wa Wamisri kama alivyoahidi?
-Ndiyo.



-Adhabu ya Mungu kwa dhambi ni kifo.

-Mungu ataadhibu dhambi yote.
-Mungu ataadhibu dhambi yote kwa kifo.

-Mungu anapoamua kuwadhibu dhambi, hakuna atakayeepuka.

-Je, wazaliwa wa kwanza wa Israeli walikufa?
-La.

-Je, kwa nini hakuna mzaliwa wa kwanza wa Israeli aliyekufa?

-Kwa sababu Waisraeli walimtii Mungu na kuweka damu katika milango yao.

-Kama vile kondoo asiye na mawaa alikufa kwa niaba ya Isaka, ndivyo kondoo asiye na mawaa alikufa kwa niaba ya wazaliwa wa kwanza wa Israeli.

-Je, kwa sababu Waisraeli walimtii Mungu, Mungu alitimiza ahadi yake na kupita juu ya nyumba za Israeli?
-Ndiyo.

-Mungu alikumbuka ahadi yake ya kuwaongoza Israeli kutoka Misri na kutoka utumwani.

-Mungu alikumbuka ahadi yake ya kumtuma Mwokozi kupitia kwa Ibrahamu na Waisraeli.

-Waisraeli walikuwa uzao wa Adamu na Hawa kama vile

Wamisri.

-Waisraeli walizaliwa katika dhambi kama vile Wamisri.

-Waisraeli walitenda dhambi na walistahili kufa kama vile Wamisri.

-Ni neema ya Mungu pekee iliyowaokoa Waisraeli.
-Ni neema ya Mungu inayookoa mtu yeyote.

-Baada ya wazaliwa wa kwanza wa Wamisri na wa Farao kufa, aliamua kufanya nini?

Tusome Kutoka 12:31-36

31-Akawaita Musa na Haruni usiku, akasema, Ondokeni tokeni katika watu wangu, ninyi na wana wa Israeli; enendeni, kamtumikieni Bwana kama mlivyosema.
32-Twaeni kondoo zenu na ng'ombe zenu kama mlivyosema, enendeni zenu, mkanibariki mimi pia.
33-Wamisri nao wakawahimiza watu, kuwatoa katika nchi kwa haraka, maana walisema, Tumekwisha kufa sote.
34-Watu wakauchukua unga wa mikate yao kabla haijatiwa chachu, na vyombo vyao vya kukandia wakavitia ndani ya nguo zao mabegani.
35-Wana wa Israeli wakafanya kama neno lile la Musa; wakataka kwa Wamisri vyombo vya fedha na vyombo vya dhahabu, na mavazi.
36-Bwana akawajalia kupendelewa na Wamisri hata wakawapa kila walichokitaka. Nao wakawateka Wamisri nyara.



-Usiku huo, Farao alimuita Musa na kuwaruhusu Waisraeli kuondoka.

-Farao alidhani kuwa angeweza kupigana na Mungu.

-Farao alidhani kuwa angeweza kupigana na Mungu na amshinde Mungu.

-Shetani alidhani kuwa angeweza kupigana na Mungu na amshinde Mungu.

-Hakuna anayeweza kumshinda Mungu.
-Hakuna anayeweza zuia kazi ya Mungu.

-Mungu atawaokoa wale watakaofuata njia ya Mungu.
-Mungu atawaaribu wale watakaofuata njia yao.

Tusome Kutoka 12:51

51-Ilikuwa siku ile ile moja, Bwana akawatoa wana wa Israeli katika nchi ya Misri kwa majeshi yao.

-Mungu alitimiza ahadi yake na kuwongoza Waisraeli kutoka Misri.

-Je, Farao anaweza pigana na Mungu na ashinde?
-La.

-Je, yeyote anaweza pigana na Mungu na ashinde?
-La.